

**BENKI KUU YA TANZANIA**  
16 Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Simu: +255 26 2962586

Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



**BANK OF TANZANIA**  
16 Jakaya Kikwete Road  
P.O. Box 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Phone: +255 26 2962586

Email: botcommunications@bot.go.tz

## **Taarifa ya Kamati ya Sera ya Fedha**

Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania imefanya kikao chake cha kawaida cha 215 tarehe 23 Julai 2021 kujadili utekelezaji wa sera ya fedha, na kupitia mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa ndani na wa dunia. Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwezi Mei na Juni 2021, uliowezesha kuendelea kuwepo kwa ukwasi wa kutosha katika mabanki. Aidha, mwenendo wa riba katika soko la fedha uliendelea kuwa tulivu na katika viwango vya chini. Hali hii imeendelea kuweka mazingira ya kuongezeka kwa kiwango cha mikopo inayotolewa na mabanki kwa sekta binafsi na kupungua kwa riba za mikopo.

Kuhusu uchumi wa ndani, Kamati imeendelea kusesitiza kwamba kuimarika kwa mazingira ya uchumi wa dunia kutachochea kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi nchini, hasa ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na uchumi wa dunia. Mfumuko wa bei nchini umeendelea kubaki katika kiwango cha chini, ukiwa ndani ya lengo la kati ya asilimia 3 hadi 5. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa wa kiwango cha chini, licha ya ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha sanjari na malengo ya nchi na ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kuchangia utulivu wa thamani ya shilingi. Kamati imesisitiza umuhimu wa kuendelea kutanua wigo wa masoko ili kuongeza thamani ya bidhaa za ndani zinazouzwa nje ya nchi.

Aidha, Kamati imeona kuwa kasi ndogo ya ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi katika mwaka 2020/21 imechangiwa na athari hasi za UVIKO-19 katika shughuli za biashara. Aidha, Kamati imetambua kwamba kuimarika kwa uchumi wa dunia pamoja na hatua za ziada zinazotarajiwa kuchukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa lengo la kuweka mazingira ya kupungua kwa riba za mikopo, kutapelekea kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Kwa kuzingatia hayo, Kamati ya Sera ya Fedha imeendelea kuridhia utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika kipindi cha mwezi Julai na Agosti 2021.

**Gavana**  
**Benki Kuu ya Tanzania**